

## **NAFASI YA KEJELI KATIKA TAMTHILIA YA KAPTULA LA MARX: SILAHA MUHIMU YA KUFIKIRISHA, KUKEBEHI NA KUFICHUA UOZO**

*Saade Mbarouk*

*Baraza la Kiswahili la Zanzibar – Tanzania/Zanzibar*

*[khasma10@yahoo.com](mailto:khasma10@yahoo.com)*

### **Ikisiri**

*Kejeli ni mbinu muhimu ya kifani inayochangia uandishi bora wa kazi za fasihi. Katika tungo bunilizi za fasihi andishi ya Kiswahili, kejeli ilianza kutumika katika karne ya 20, wakati waandishi wa mwanzo wa kazi bunilizi walipoonesha uwezo wao wa uandishi uliobeba vionjo makini vya kiujumi ili kuifikirisha hadhira na kuweka wazi matatizo ya jamii. Makala hii inalenga kuiangalia nafasi ya kejeli kama silaha muhimu ya kufikirisha hadhira, kukebehi na kufichua uozo unaotendeka ndani ya jamii. Uchambuzi wa makala hii umeongozwa na Nadharia ya Semiotiki iliyoendelezwa na mwanamuundo maarufu, Roland Barthes. Data zilikusanywa kupitia njia ya maktabani na uwandani kwa kutumia njia ya udurusu wa matini na mijadala ya makundi. Data zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya kitaamuli. Makala hii imebainisha na kufafanua nafasi ya kejeli zilizojitokeza katika tamthilia ya Kaptula la Marx katika miktadha ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii ambazo ni kukosoa, kukebehi, kudharau waovu, kufichua na kukemea uovu unaofanyika katika jamii, kama vile uifisadi, unyanyasaji, ubaguzi na kuburudisha hadhira.*

### **1.0 Utangulizi**

Kueleweka kwa maana ya kejeli ni muhimu ili kujenga mwelekeo mahususi wa makala hii. Hii ni kutokana na kuwapo kwa ufafanuzi wa kejeli unaotofautiana kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali walioshughulikia dhana hii kama Kierkegaard (1977) Cuddon (1991), Baldick (2001), Mbatiah (2001), Wamitila (2002) na Senkoro (2011). Kwa mfano, Baldick (2001) anasema, kejeli ni mawazo ya kiucheshi yanayokinzana, ambapo

kauli ya uwazi au tukio huonekana kuficha kitu ndani ya muktadha au tukio, kwa lengo la kuyapa umuhimu mbalimbali. Mawazo ya Baldick (keshatajwa) yanajenga hoja ya msingi, kwani yanaonesha namna kejeli zinavyohitaji kupewa umuhimu na kuzitafakari kwa umakini, kutokana na kuwa huweza hubeba matukio ya msingi yenye kuweka wazi matatizo yetu kwa lengo la kuijenga jamii. Naye Cuddon (1991) akimnukuu Amiel (1883) anaeleza kwamba, kejeli zimezuka kutokana na maisha ya kiubwege. Kwa ujumla Cuddon na Amiel (wameshatajwa) wanakubaliana kuwa kejeli ni ulimbwende. Mawazo yao yanatuonesha kuwa kejeli inatokana na kuwepo kwa ubwege. Hivyo, kazi ambazo ni za kiubwege hubeba kejeli nyingi ambazo hulenga kujenga uzuri wa kazi hizo kisanaa ili kuvutia na kuweka wazi uozo au kukosoa jamii. Vilevile, Mbatiah (2001) anafafanua dhana ya kejeli kwa mtazamo finyu. Anaeleza kuwa, kejeli ni maneno yanayotumiwa katika mazungumzo; matamshi kama hayo huwa ni ya kuchoma, kukata na kutia uchungu. Maelezo ya Mbatiah yanaonesha kuwa moja ya dhima ya kejeli ni kutia uchungu kwa anayeambiwa. Hata hivyo, maelezo yake yanakinzana na baadhi ya wataalamu, ambao wanaona kuwa sio kila kejeli inatia uchungu. Mara nyingine anayekejeliwa hasikii mwenyewe au mara nyingine kejeli huwa ni mzaha na huchekesha tu. Kwa mfano, Ponera (2014) anafasili kwamba futuhi ni mchezo unaojumuishia vichekesho na kejeli ambazo hatimaye, huibua furaha kwa wahusika.” Dondoo hili linasisitiza kuwapo kwa dhima chanya ya kejeli ambayo ni kuchekesha. Dondoo hili linaonesha kuwa kuna upande mwingine wa matumizi yake. Kwa upande wa mtafiti, anafafanua dhana ya kejeli kuwa ni tamathali inayozungumza jambo kinyume na kilichokusudiwa au uhalisi wa tukio ama hali iliyopo, katika muktadha maalumu unaokusudiwa na mwandishi msemaji au mzungumzaji, kwa lengo la kufikirisha, kukebehi, kuweka wazi matukio yanayotendeka katika jamii na kuburudisha. Kwa ujumla, fasili hizi zinaweka wazi mambo ya msingi katika kejeli, kama matumizi ya unyume, umuhimu wake katika uandishi wa kazi za fasihi na jamii. Kauli ambayo inashadidiwa na Dib (2019); anasema, “Wanaubwege hutumia mbinu za tamathali za semi nyingi kwa lengo la kuisisitiza ubwege katika tamthilia hizo”. Zana za kibalagha au tamathali za semi hutumiwa kwa kila kazi za thieta ya ubwege. Miongoni mwa hizo ni mafumbo, kweli kinzani, tashtiti,

dhihaka na iliyo muhimu zaidi ni kejeli. Naye Mrikaria (2010) anaeleza kuwa mbinu ya kejeli huonesha vituko na mbwembwe nyingi zinazopelekea kufurahisha, kuteta, kufunza na kuonya kiasi kwamba si rahisi kuvitambua, kuvikubali au kuvikataa ndani ya jamii.

Matumizi ya kejeli katika uga wa kitaaluma inaaminika yalianza tangu karne nyingi zilizopita, toka enzi za ustawi wa mataifa ya Ulaya. Huu ni wakati ambao wanafalsafa maarufu wa Kiyunani, Plato na Aristotle walitumia mbinu ya kejeli katika dayalojia zao za kifalsafa kwa lengo la kuwafanya watu wajitambue, na ndipo matumizi ya kejeli yalianza kupata mtazamo mpya. Toka wakati huo, kejeli ilianza kuwa mbinu ya kisanaa iliyotumiwa na waandishi wa kazi mbalimbali za fasihi ulimwenguni. Wanafalsafa hao wa kale walianza kutumia kejeli katika dayalojia zao tofauti, na ndipo ilipoibuka dhana ya “Dayalojia ya Kiplatoniki” na “Dayalojia ya Kisokreti”. Ijapokuwa maana ya msingi ya kejeli inaonesha uhasi, katika mtazamo wa kifalsafa na fasihi kupitia Dayalojia ya Kisokreti, inaonekana kuna tofauti. Jambo hili linadhihirika kutokana na mtazamo wa dhima iliyobeba dayalojia hizo. Hoja hii inatoa picha kuwa dayalojia za kikejeli zililenga kutathmini uwezo na ujuzi alionao mhusika mwenza katika dayalojia. Pia, zililenga kumfanya mtu ajitambue zaidi katika nafasi yake. Kejeli ni dhana yenye nguvu sana itumikayo katika tashtiti (Highet, 1962). Maelezo hayo yanakwenda pamoja na hoja ya Griswold (2002) inayosema kuwa, tunaweza kufahamu mtazamo wa kejeli kama tukiunganishwa na matarajio ya Plato ya kumweka msomaji katika maisha ya uchunguzi wake mwenyewe. Hali hii inatudhihirishia kuwa licha ya kuwa katika mazungumzo yetu ya kawaida watu wanaichukulia kejeli kuwa ni dhana hasi, katika mtazamo wa kifasihi inalingana sana na matumizi yake ya awali katika falsafa. Matumizi hayo yana lengo la kujenga hali ya uelewa na kujitambua kwa wanajamii. Kejeli huisaidia jamii kutafakari juu ya matukio mbalimbali yanayojitokeza katika kazi hizo za fasihi kwa jicho pekuzi ili kuelewa vyema jamii yao. Kwa hivyo, katika kipindi hicho kejeli kama mbinu ya kufikirisha na kuelezea fikra, ilianza kufikia katika kiwango kikubwa na kigumu. Ilichukuliwa kuwa ni mojawapo ya mbinu za kibunilizi ambayo watu mbalimbali huitumia katika kazi za fasihi. Mbinu hii

ilichukuliwa kuwa na nguvu maalumu za kitashtiti na kibalagha. Kejeli hutumiwa na waandishi kuionesha hadhira yao mazuri na maovu yaliyomo katika jamii zao.

### **1.1 Muhtasari wa Tamthilia ya *Kaptula la Marx***

Tamthilia ya *Kaptula la Marx* imeandikwa na Euphrase Kezilahabi, na kuchapishwa mwaka 1999 na *Dar es Salaam University Press*. Toleo lililotumiwa katika makala hii ni la mwaka 2010. *Kaptula la Marx* ina jumla ya sehemu sita ambazo haziko katika mtiririko wa kimfuatano. Mchezo unaanza gerezani na kisha kubadilisha mahali kwa kuonesha wako bungeni na mahakamani, ijapokuwa mandhari ni ileile ya gerezani. Katika gereza hilo, kuna wafungwa na. 1 hadi 6. Mfungwa na. 6 (Mwangaza Africanous) ndiye kiongozi kati ya wafungwa hao. Pia, kuna serikali inayoongozwa na Rais Kapera ambayo haikutajwa ni ya nchi gani. Tamthilia imeanza kwa jaribio la wafungwa walioko gerezani kukusanya habari mbalimbali kutoka nje ya gereza, baada ya kufanikiwa kutoboa tundu wakati wamo ndani ya gereza, ili waone kilichoko nje. Inaendelea kwa kuonesha tukio la Rais Kapera kusoma habari za Marx ili aweze kubadili siasa yake na kufuata siasa ya Marx, kwa lengo la kuleta maslahi kwa umma anaouongoza. *Kaptula la Marx* na shati alilolivaa lilikuwa ni kubwa mno kwake. Aliwataka mawaziri wake wamuangalie amefanana na nani. Lakini walishindwa kupata jibu sahihi ikiwa alikuwa amefanana na Marx, Mao au mwingine. Hata hivyo, Rais Kapera na mawaziri wake waliamua kuvaa vazi hili. Kisha, wanaamua kuondoka na mavazi yao kuelekea kwenye nchi ya haki na usawa. Njiani wanakutana na Jitu, jina lake halisi ni Korchnoi Brown. Rais Kapera anamuomba amuelekeze njia. Maelekezo ya Brown kuhusu safari hiyo, yanaonesha vikwazo vingi. Pia, baada ya kuwaona baadhi ya mawaziri wa Rais Kapera, Brown aliitilia shaka safari ya kufika huko walikokusudia, ambapo kweli walishindwa kufika. Mawaziri wengine wanakufa njiani na wengine wanajeruhiwa. Wakati huohuo, wafungwa gerezani wanafanya majadiliano kuhusu siasa za nchi zao. Mwangaza Africanous anasoma ujumbe wa viongozi wa nchi za Afrika, huku akikataa siasa zao. Katika sehemu ya mwisho, wafungwa waliotoka gerezani

wakishirikiana na waziri wa kike wanafanya mapinduzi. Kicheko cha Brown kinafunga tamthilia.

## 1.2 Nadharia ya Semiotiki

Kwa mujibu wa Mulokozi (2017), Semiotiki au Semiolojia ni nadharia inayozingatia ishara na uashiriaji. Nadharia hii inatokana na vyanzo viwili vikuu. Nadharia ya Kimuundo ya mwanaisimu wa ki-Swiz, Ferdinand de Saussure (1857- 1913) na Nadharia ya Semiotiki ya Mmarekani, Charles S. Peirce (1839- 1914). Nadharia hii imepata ushawishi muhimu kupitia wanaumuundo. Nadharia ya Semiotiki iliendelezwa na Julia Kristeva (Baldik, 2001). Naye Wamitila (2002) anaeleza kuwa, mawazo ya wanamuundo yamekuwa na athari kubwa katika uhakiki wa ishara na uashiriaji katika kazi za kifasihi. Miongoni mwa misingi muhimu ya nadharia hii ni ule ulioanzishwa na Roland Barthes (1915-1980) ambao ni “msimbo”. Msimbo ni miongoni mwa nguzo kuu za Nadharia ya Semiotiki. Barthes (keshatajwa) alifafanua misimbo hiyo kama ifuatavyo:

- (a) Msimbo wa matukio: Huu unahusu namna matukio yanayopatikana katika hadithi yanavyofuatana na jinsi msomaji anavyounda na kuelewa msuko wa kazi ya kifasihi, kwa kuangalia jinsi matukio hayo yanavyofuatana kiathari au kinasaba.
- (b) Msimbo wa kihemenitiki: Msimbo huu unahusu taharuki na usimulizi na kwa hivyo huitwa msimbo wa kusimulia au msimbo wa kutamba hadithi na unaweza kufumbatwa kwenye jina la kazi.
- (c) Msimbo wa ki-seme: Huu hueleza elementi nasibishi za kisemantiki ambazo hutupatia picha ya mhusika fulani wa kifasihi.
- (d) Msimbo wa kiishara: Huu unahusishwa na namna wasomaji wanavyofumbua maana za ishara katika kazi za kifasihi.
- (e) Msimbo wa kiurejelezi: Huu hujengwa kutokana na viashiria vya kiutamaduni ambavyo vinarejelewa katika kazi za kifasihi. Huhusisha matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka miongoni mwa wasomaji na hivyo kuipa kazi fulani nguzo ya kiutamaduni.

Nadharia hii ilimuongoza mtafiti kukusanya, kuchanganua na kufasili kauli za kejeli zilizojitokeza katika tamthilia hii. Kwani kauli za kejeli hizo nyingi

zilionekana kutumia ishara. Misimbo kama vile wa kihementiki, kiurejelezi, kiseme na kiishara imetumika katika uchanganuzi wa data. Nadharia ilisaidia vyema kukamilisha malengo ya utafiti uliofanyika kutokana na kuwa mawazo yaliyobainishwa yanahusiana na malengo ya utafiti uliofanyika kama kubainisha na kufafanua kejeli na kuonesha nafasi ya kejeli hizo katika miktadha tofauti iliyobainishwa.

### 1.3 Methodolojia

Utafiti uliozaa makala hii ulitumia usampulishaji lengwa kupata watoa taarifa waliohitajika. Mbinu zilizotumika katika mchakato wa ukusanyaji wa data ni ya maktabani na uwandani. Data ilikusanywa kupitia njia ya udurusu matini na mjadala wa vikundi. Mwongozo wa maswali uliotumika ulisaidia kupata mawazo na mitazamo ya watu katika kuzibainisha kejeli zilizojitokeza katika tamthilia iliyotumika. Mtafiti alikuwa makini katika kubainisha kejeli, kuchambua na kutafsiri ishara zilizojitokeza katika kejeli zilizobainishwa katika tamthilia ya *Kaptula la Marx* na kuzifafanua. Makala hii iliongozwa na Nadharia ya Semiotiki katika uchanganuzi wa data zilizokusanywa. Katika nadharia hii misimbo iliyotumika katika uchambuzi wa data ni misimbo wa kiurejelezi, msimbo wa kiseme, msimbo wa kihementiki, msimbo wa kina. Kwa kuwa data zinazochambuliwa kupitia mkabala wa kitaamuli huweza kutafsirika kwa namna tofauti kulingana na mtazamo na muktadha uliotumika.

### 1.4 Chimbuko la Kejeli Duniani

Chimbuko la kejeli linatokana na neno *Eiron*. Neno hili linaturudisha nyuma hadi zama za kale, hasa katika wakati wa komedi za Kigiriki. Eiron ambaye alikuwa ni mhusika maarufu alitumiwa na mwanafalsafa ya Kigiriki, Aristotle, katika kazi yake maarufu *Nicomachean Ethics*, ambayo inawasilisha msingi wa kejeli katika drama. Kupitia mhusika huyo Eiron ndipo lilipoibuliwa neno kejeli (*irony*). Hivyo, historia ya kejeli na historia ya drama au michezo ya jukwaani inaonekana kuwa na mfungamano na kejeli. Katika kipindi cha sasa pia kumekuwa na madai kuwa hata asili ya kejeli na thieta zina mshikamano wa karibu sana, na kila moja ina umuhimu kwa nyenziwe, yaani zinakamilishana.

Maelezo hayo yanakwenda pamoja na hoja ya Griswold (2002) inayosema kuwa, tunaweza kufahamu mtazamo wa kejeli kama tukiunganishwa na matarajio ya Plato ya kumweka msomaji katika maisha ya uchunguzi wake mwenyewe. Hali hii inatudhihirishia kuwa licha ya kuwa katika mazungumzo yetu ya kawaida watu wanaichukulia kejeli kuwa ni dhana hasi, katika mtazamo wa kifasihi; inalingana sana na matumizi yake ya awali katika falsafa. Matumizi hayo yana lengo la kujenga hali ya uelewa na kujitambua kwa wanajamii. Kejeli huisaidia jamii kutafakari juu ya matukio mbalimbali yanayojitokeza katika kazi hizo za fasihi na kuitazama jamii kwa jicho pekuzi ili kuielewa vyema.

Naye Dib (2019) anaeleza kuwa mtumizi ya kejeli katika drama na thieta yalianza tokea mwanzoni mwa kipindi cha kiulimbwende. Huu ni wakati ambao watu walianza kuangalia na kushuhudia uhusiano kati ya kejeli na thieta (michezo ya jukwaani). Anaendelea kusema kuwa, mbinu ya kejeli ilipata matumizi makubwa mwishoni mwa karne ya 17 au mapema katika karne ya 18. Katika kipindi hicho, kejeli ilichukuliwa kuwa ni mbinu mojawapo ya kibunilizi ambayo watu waliitumia katika kazi za fasihi. Wamitila (2010:402) anaeleza kuwa kejeli ni mojawapo ya mbinu zinazotawala maongezi yetu hasa kutokana na uwezo wake wa kufichua hisia, maoni na mitazamo yetu sahihi. Hivyo, ni wazi kuwa kejeli ina nafasi pana na muhimu katika nyuga mbalimbali za maisha ya wanajamii. Kwa hivyo, katika kipindi hicho kejeli kama mbinu ya kufikirisha na kuelezea fikra, ilianza kufikia katika kiwango kikubwa na kigumu. Ilichukuliwa kuwa ni mojawapo ya mbinu za kibunilizi ambayo watu mbalimbali huitumia katika kazi za fasihi. Mbinu hii ilichukuliwa kuwa na nguvu maalumu za kitashtiti na kibalagha. Kejeli hutumiwa na waandishi kuionesha hadhira yao mazuri na maovu yaliyomo katika jamii zao.

### 1.5 Uhusiano wa Kejeli na Tamthilia

Kejeli ina uhusiano wa karibu na tamthilia. Kuna wataalamu mbalimbali waliojadili kuhusu uhusiano wa kejeli na tamthilia. Mueke (1971), Sedgewick (1935), na Dib (2019) wanazungumzia uhusiano uliopo kati ya kejeli na drama. Kwa mfano, Sedgewick (keshatajwa) anadokeza kuwa, thieta yenyewe ni aina ya kejeli iliyofumbatwa humo. Wataalamu hao wanaona kwamba, ni suala lisilowezezana kutenganisha kejeli kutoka katika tamthilia. Wanaamini kwamba tamthilia na kejeli vina sifa muhimu za pamoja zilizofanana katika kuwapo kwake. Wakiwa na maana kwamba vitu vilivyomo kati ya kejeli na thieta vinahusiana katika msingi maarufu wa mantiki ya unyume. Naye Wilson (2014) anathibitisha uhusiano wa wazi usiopingika wa kejeli na drama, pale alipoandika katika utangulizi wa kitabu chake *The Theatre Experience*. Alieleza kuwa kejeli ni kauli inayosemwa ambayo matumizi yake hukusudia kinyume na hali halisi. Kejeli ni zana inayofaa zaidi katika thieta na huonekana kwa kiasi kikubwa zaidi katika tamthilia. Anaendelea kusema kuwa thieta ni mandhari rutubishi katika utekelezaji na uwasilishaji wa kejeli, na bila shaka kuna upekee kuhusiana na kejeli unaoifanya istahiki katika thieta. Hoja hii inatoa maelezo ya jumla kuhusu umuhimu wa kejeli katika tamthilia. Pia, kuonesha kuwa licha ya kuwa kuna matumizi ya vipengele vingine vya tamathali za semi, kejeli ndiyo inayojenga msingi wa tamthilia, hasa za ubwege.

Maelezo haya ni muhimu katika makala hii kwa sababu yalituelekeza kuwa, kejeli ina nafasi ya upekee katika tamthilia. Pamoja na mwanga tulioupata katika hoja hiyo, bado ilituachia swali muhimu lililohitaji kupatiwa jibu katika utafiti wetu. Majibu ambayo yalikuwa nje ya majibu ya Wilson (keshatajwa); je, kejeli hiyo huwa na nafasi gani hasa katika tamthilia za ubwege? Swali hili linajibiwa vyema katika sehemu zinazofuata katika makala hii.

Aidha, kejeli katika tamthilia hujikita katika kushughulikia nafasi mbili tofauti katika jamii. Kejeli katika tamthilia hujikita kuonesha mambo ya kawaida ama mepesi katika jamii, pia, masuala mazito kama ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Kejeli zote hizi husimama kuwa ni silaha



muhimu ya uandishi yenye lengo la kukosoa na kurekebisha kwa lengo la kutoa tiba kwa jamii inayougua maradhi sugu kama vile ufidiaji, usaliti na ubinafsi. Kejeli nyingine huwa wazi na nyingine ni fiche, lakini zote zinapotumika katika kazi ya fasihi huhitaji kufikiriwa kwa umakini. Kwa mnasaba huo, kejeli hutoa ushawishi kwa msomaji wa kazi ya fasihi kuchunguza kwa umakini elementi mojambo katika matini ili aweze kufahamu kinachoelezwa na mwandishi na ndipo anapoweza kuihusisha na jamii inayomzunguka. Maelezo haya yalikuwa ni dira muafaka iliyosaidia vyema katika makala hii, kwa sababu yamekuwa ni kiunzi madhubuti kilichomwongoza mtafiti kuzifasiri kejeli zilizotumika katika tamthilia iliyochunguzwa. Pia, yametoa mchango muhimu uliosaidia kuonesha namna mwandishi anavyojenga kejeli na kumuongoza kupata mwelekeo sahihi wakati alipochambua data zake na kuchunguza nafasi ya kejeli katika tamthilia hii ya *Kaptula la Marx*.

### **1.5.1 Matumizi ya Kejeli katika Fasihi za Kiswahili**

Kwa mujibu wa Mrikaria (2010) katika fasihi ya Kiswahili mbinu ya kejeli hupatikana katika mawanda mapana na ya aina mbalimbali. Kuna kejeli ambazo zinapatikana zaidi katika utanzu wa tamthilia kuliko katika riwaya. Kundi la kwanza ambalo ni asilia katika fasihi lenye kubeba mzigo mkubwa wa kejeli ni fasihi simulizi. Kundi hili lina tanzu zilizogawanyika katika makundi makuu manne, yaani hadithi, ushairi, semi na sanaa za maonesho. Wamitila (2003) anasema kuwa kejeli ya kiusemi inaelezwa kama ni kejeli ya msingi sana na hutokea pale ambapo pana mkinzano fulani baina ya kile kinachosemwa na uhalisia wenyewe. Anasema kwamba, uelewaji wa kejeli ya kiusemi huhitaji msemaji na msikilizaji au hadhira kuwa na hisia au mwelekeo fulani kuhusu mada inayozungumziwa. Maneno ya Wamitila yana ukweli ndani yake kwa sababu si rahisi kwa jamii yenye utamaduni usiofanana na jamii nyingine kuelewa barabara semi za kejeli sawasawa na jamii husika. Khatib (1986) anaeleza kuwa katika Afrika Mashariki kejeli imetumika sana hasa katika fasihi simulizi kama vile nyimbo, mashairi, tenzi, methali, vitendawili, utani na nyinginezo. Khatib anakiri kuwa, tamathali za semi zikiwemo kejeli hutumika katika mazingira ya Waswahili; zinabuniwa katika maisha ya kila siku ya watu kama katika misiba, mizungu

na kunga za kuwafunza wari, gulioni na katika pungo za kupunga pepo na mashetani.

Naye Mrikaria (2010) anashadidia hoja hii kwa kusema kuwa, kwa upande wa tungo bunilizi za fasihi andishi ya Kiswahili, kejeli ilianza kutumika katika karne ya 20, wakati waandishi wa mwanzo wa kazi hizi bunilizi walipoonesha uwezo wao wa uandishi uliobeba vionjo makini vya kiuajumi kama Shaaban Robert, ambaye ni kielelezo dhahiri cha uandishi wa nathari za kikejeli katika fasihi ya Kiswahili. Hoja hii pia inaungwa mkono na Senkoro (2011) aliyefafanua namna matumizi ya kejeli katika fasihi ya Kiswahili, anasema kuwa:

Kabla ya miaka ya katikati ya sabini na themanini, tulikuwa na waandishi wachache sana watumiao kejeli kama vile Shaaban Robert, ambaye alikuwa maarufu kama Shakespeare wa Tanzania. Katika miaka ya hamsini, Shaaban Robert aliandika *Kusadikika* na *Kufikirika* kwa kutumia njia ya kejeli na kuonesha madhila makubwa yaliyotokana na ukoloni Barani Afrika (uk. 29).

Senkoro na Khatib wamejadili matumizi ya kejeli kwa ujumla katika fasihi ya Kiswahili na kutuachia pengo la kulichunguza katika utafiti wetu, kwa sababu, wataalamu hao hawakufafanua kwa kina kuhusu kejeli. Ingawa maelezo hayo yalisaidia kutoa mwanga kuhusu matumizi ya kejeli, yalikuwa nje ya mwega ambao sisi tuliazimia kuuchunguza. Hivyo, yametoa mwanya mzuri kwa mtafiti kuchunguza nafasi ya kejeli na namna kejeli hizo zilivyotumika katika miktadha tofauti katika tamthilia hii. Pia, hawakufafanua kwa uwazi kwa namna gani kauli za kejeli zinavyosaidia hadhira kufikiri kwa kina kuhusu matukio ya kijamii. Wametaja tu kwa ujumla na hawakuweka wazi na kuonesha mifano na mazingira gani hasa kejeli hizo zimetumika na kuacha mwanya unaotakiwa kuzibwa. Hivyo, kutuhamasisha kuchunguza kejeli katika tamthilia ya *Kaptula la Marx*. Maoni kama hayo yametiliwa mkazo na Mrikaria (2010). Anaeleza kuwa katika fasihi ya Kiswahili zipo kazi nyingi ambazo zimejikita katika dhana za kejeli. Katika kazi hizo kejeli ilitumika kuelezea historia ya Tanzania

kabla ya uhuru, baada ya uhuru, baada ya Azimio la Arusha na hata hivi sasa katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia. Kejeli ni mbinu pana ambayo huchukua nafasi kubwa na kutoa mchango wake si katika mazungumzo tu bali pia katika utoaji wa mawazo yetu ya kila siku. Katika fasihi mbinu ya kejeli imetumiwa na inaendelea kutumiwa na waandishi kuiwezesha hadhira au wasomaji wafikirie kwa undani suala linaloongelewa ili waweze kupata ujumbe uliokusudiwa kufikishwa kwao. Kutokana na mantiki hiyo, waandishi huichora kejeli kwa kutumia fikra tofauti kwa kutumia kazi zao za fasihi. Kejeli hizo huzijenga katika sura mbalimbali kwa kutumia, ishara, tashtiti, au jazanda. Pia, taswira, ujumbe na mpangilio wa maudhui ya kazi zao vimelenga katika kuwasema watu ambao wamebeba dhamana kubwa kwa jamii zao. Hivyo, kwa mantiki hiyo, makala hii imebainisha na kufafanua namna mwandishi wa *Kaptula la Marx* alivyotumia kejeli katika miktadha tofauti. Makala hii imejikita katika kuangazia na kuweka wazi namna kejeli ilivyo na nafasi ya kufikirisha hadhira husika, inavyokebehi na kufichua uozo uliopo ndani ya jamii.

## **1.6 Nafasi ya Kejeli katika Tamthilia ya *Kaptula la Marx***

Katika makala hii, miktadha tofauti imebainishwa kulingana na mwelekeo wa mazungumzo yalijojitokeza katika tamthilia hii. Miongomi mwake ni muktadha wa kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii. Kupitia miktadha hiyo, makala imebainisha nafasi mbalimbali zilizojitokeza katika miktadha hiyo.

### **1.6.1 Nafasi ya Kejeli katika Muktadha wa Kisiasa**

Matumizi ya kejeli yamejitokeza kwa kiasi kikubwa katika tamthilia ya *Kaptula la Marx*. Katika tamthilia hii, kuna kejeli nyingi zinazoonisha hali ya siasa katika bara la Afrika. Kwa mfano, kejeli imebainika kwa kuangalia kirai ‘Kaptula la Marx.’ Kwa kuzingatia matazamo wa nje, tunapata maana kuwa, kaptula hili linamilikiwa na Marx. Tunapoingia ndani zaidi tunaona kuwa Kaptula la Marx ni kichwa cha anuani ya tamthilia iliyotumika kiishara. Neno ‘Kaptula’ ni aina ya suruali ambayo ni fupi kuliko suruali za kawaida, ambayo haifiki chini katika vifundo vya miguu; mara nyingi huishia kwenye magoti au kwenye miundi, ilhali ‘Marx’ ni jina la mtu.

Majina hayo yanapowekwa katika kirai na kuwa ‘Kaptula la Marx’ bado inaonekana yanahitaji ufafanuzi wa ziada ili ipatikane taarifa iliyokamilika kulihusu kaptula hilo. Hivyo, msomaji anaposoma tu anuani ya kazi hii lazima atakuwa na hamu ya kuelewa na kujiuliza maswali kama, kwa nini Kaptula la Marx? Lina nini hilo kaptula? Mazungumzo ya wahusika ndiyo yatakayomfanya msomaji kuelewa kwa nini mwandishi ametumia anuani hiyo. Anuani hiyo ya ‘Kaptula la Marx,’ humpa msomaji taharuki fulani ya kutaka kujua kupitia usimulizi wa hadithi iliyomo katika kazi hiyo. Hivyo, msomaji hulazimika kufikiri kwa makini na kuhusisha viashiria hivyo na matukio yaliyomo ndani ya jamii yake.

Kutokana na muktadha huo, viashiria vilivyotumika, yaani ‘Kaptula’ na ‘Marx’ tunaweza kusema kuwa vinaashiria uigaji wa mtindo wa uongozi na utawala unaoambatana na mfumo wa kisiasa wa kigeni. Siasa inayotokana na usuli wa mataifa makubwa ya Mashariki yaliyokuwa na nguvu za kisiasa. ‘Marx’ jina lililotumika kiishara, lililotumika kumfananisha mwanafalsafa wa Kijerumani aliye na asili ya Kiyahudi, aliyeanzisha Nadharia ya Umaksi, ili kuonesha uhusiano wa kisiasa na kiuchumi baina ya makundi yanayopingana kati ya mabepari na wafanyakazi. Simon (2014) anashadidia kuwa anuani *Kaptula la Marx* imetumika kusimamia kejeli iliyojengwa na mwandishi, kukebehi uigaji wa mfumo wa kisiasa. Pia, inawakejeli watu waliofuata mkumbo kuiga nadharia na mfumo wa kisiasa na kiuchumi wa Karl Marx na Freidrick Engels. Mifumo inayoendana na misingi ya siasa ya ujamaa na kikomunisti, bila hata kuelewa jinsi inavyoweza kutekelezwa kwa manufaa, na kama kweli inaweza kutekelezeka katika mazingira ya Afrika.

Katika muktadha huu, yumkini, kuwa mwandishi anamtumia kiongozi huyu, Rais Kapera aliyejivisha kaptula la Marx, kuashiria taifa la Tanzania hususan tunaporejela katika miaka ya 1970– 80, wakati lilipojaribu kutekeleza mfumo wa siasa ya ujamaa, ambao mwishowe uliporomoka. Wamitila (2010) anaeleza kuwa Kaptula la Marx ni anuani ya kiishara za kifaharasa, inayopaswa kufasiriwa ili ieleweke. Vichwa vya aina hii huhusisha msimbo wa kihementiki ambapo usimulizi wa hadithi huweza

kufumbatwa kwenye anuani ya kazi ya fasihi husika. Hivyo, kwa vile mwandishi ni Mtanzania, anaonekana aliufahamu vizuri na kuona athari za mfumo huo. Aliona namna ulivyoanza, wakati na sababu za kutetereka kwake na namna alivyoshuhudia kuporomoka kwa mfumo huo. Hivyo, mwandishi ametumia kejeli hii ya kitashtiti kudhihaki na kukebehi kutokufanikiwa kwa mfumo huo.

Vilevile, kejeli nyingine imebainika kupitia majibu ya Waziri wa Utamaduni na Waziri wa Ulinzi wa zamani. Kezilahabi, anaonesha namna Waziri wa Utamaduni anavyotoa majibu ambayo hayana msingi wakati alipotakiwa kueleza juu ya maendeleo aliyofikia katika wizara yake. Kama inavyoonekana katika dondoo lifuatalo:

Waziri wa Utamaduni...Timu yetu ya taifa imetolewa na timu ya taifa ya jirani zetu. Kuhusu mambo ya kale tumetoa pesa kutengeneza upya mapango ya watu wa kale. Na wataalamu wetu wanaendelea kuchimba mafuvu ... Kuhusu mila hivi sasa tunafanya uchunguzi juu ya nyoka katika ngoma, uchawi na talaka. Kuhusu lugha wananchi wanaonekana wana mwamko mkubwa kisiasa. Wanaimba ngonjera na mashairi juu ya ujamaa, tena yale yenye vina (uk. 10).

Ripoti ya waziri huyo inadhihirisha kejeli aliyotumia mwandishi juu ya Waziri wa Utamaduni. Maelezo yote yanalenga kuonesha namna waziri huyo alivyoshindwa kutekeleza majukumu yake. Tunaporejelea msimbo wa kiurejelezi, viashiria vilivyotumika katika dondoo hili vinatujaza juu ya kushindwa kwa utekelezaji wa majukumu ya waziri huyo. Kwa mfano, viashiria hivi vinatupatia maana tofauti. Yumkini, kauli ya mwandishi inayosema, “wanaimba mashairi juu ya ujamaa” ina maana kuwa, wanafuata tu mfumo huu kikasuku kwa kuwa hawaelewi asili na misingi ya ujamaa. Pia, kauli “tena yale yenye vina” tunapoihusisha na mashairi na vina, inaturejesha nyuma katika mgogoro wa ushairi, kati ya mashairi ya

kimapokeo na ya kimamboleo. Nguzo hiyo ya utamaduni inatufanya tuelewe kilichojitokeza miaka ya sabini, ambapo kambi mbili za washairi zilipingana. Hivyo, hali hii inaonesha namna mwandishi anavyokejeli kwa kuona kuwa, utekelezaji wa siasa ya ujamaa uliofanyika ulikuwa wa kikasuku. Kama ilivyo katika kanuni hizo za utunzi wa mashairi, mara nyingine watunzi huweza kutumia neno ambalo si muhimu ilimradi aweke sawa urari wa vina tu. Pia, elementi hizo zimetuwezesha kunasibisha na utendaji mbovu wa waziri huyo. Ukitazama kwa umakini maelezo katika dondoo hili unaweza kujiuliza, je, mambo anayoyaeleza waziri yana umuhimu gani katika maendeleo ya nchi?. Kweli ni mambo ya msingi katika kuisaidia nchi kufika kwenye usawa na demokrasia?. Mambo hayo yangesaidia vipi kufikia Ujamaa wa Kiafrika. Hivyo, ni dhahiri kuwa mwandishi ametumia kejeli kushutumumu ubaya wa baadhi ya viongozi ambao hawawajibiki katika kazi zao.

Pia, kejeli imejitokeza kupitia mhusika, Rais Kapera. Mwandishi alitumia kejeli kubainisha matendo ya Waziri wa Utamaduni yanayoonesha kuwa hana maadili na heshima kwa Rais wake, kama dondoo lifuatalo linavyoonesha:

Rais Kapera: Unakunywa nini ndugu. Hapa kwenu Bwana. Usiogope.

Waziri wa Utamaduni: Soda. Coca cola...

Rais Kapera: ... Je kutembea na wake za watu nao ni Utamaduni! (*Kimya*)

Waziri wa Utamaduni: (*Anatetemeka*) Ili ... ilikuwa ni bahati mbaya Mtukufu Rais (kur. 7- 8).

Kauli zinazotokana na dondoo hilo zimetuwezesha kupata picha halisi ya waziri huyo kuwa hana maadili. Kauli za Rais Kapera zinamtashtiti Waziri wa Utamaduni. Mtafiti amefasili hali hiyo kutokana na msimbo wa kiseme. Elementi nasibishi za kisemantiki zilizotumika zimetuwezesha kupata picha ya namna Waziri wa Utamaduni asivyokuwa na nidhamu. Maneno anayotumia Rais yanamshambulia waziri huyo. Hivyo, swali la Rais Kapera kwa Waziri wa Utamaduni limelenga shambulio la kumshusha hadhi waziri

na kuweka wazi uovu wake. Kama anavyohibitisha Frey (1957), tashtiti huwa na kilengwa cha shambulio ambacho hupatikana katika muktadha maalumu. Hivyo, mwandishi ametumia shambulio hilo kukosoa na kuihadharisha jamii na ufisadi huo.

Kama alivyoonekana mwanzo, Rais alitumia makaribisho mazuri. Alimkirimu waziri wake kama kwamba hana tatizo lolote juu yake, lakini akilini mwake anamramba kisogo. Baadaye, anaendeleza shambulio la kumuumiza waziri huyo kutokana na tabia mbaya aliyonayo, kwani unaporudi katika uhalisi wa mambo, ni vigumu sana Rais kuwa na mlahaka mzuri na mtu kama huyo. Unapozingatia muktadha uliopo kati ya waziri huyo wa kuiba mke wa Rais Kapera, ni wazi kuwa Rais alikuwa anambeza Waziri wa Utamaduni. Shambulizi la aina hii linathibitishwa na Murray katika Wamitila (2008) kuwa: “dhamira ya kimsingi ya mtumiaji tashtiti ni kuchochea kero, bezo, chuki, hasira, kinaya na hisia katika kilengwa na tashtiti hiyo”.

Pia, kejeli kama hiyo ilijidhihirisha wakati Rais Kapera alipoanza kumuuliza waziri wake maswali ya maudhi, huku akifahamu kwamba swali analomuuliza halina jibu kwa Waziri huyo. Pia, kitendo alichomuamuru akifanye ni kitu kisichowezeke bali ni njia mojawapo ya kumkejeli na kumuadhiri kutokana na matendo yake maovu. Mfano ufuatao unadhihirisha hilo:

Rais Kapera: Una ulimi wa nyoka? Lamba pua yako basi!  
(*waziri anapiga magoti akiomba radhi*) Lamba pua yako!  
(*Waziri anajaribu ulimi unakaribia lakini anashindwa udenda unamtoka*).

Waziri wa Utamaduni: (*Akijipangusa midomo*) Siwezi Mtukufu Rais. Rais Kapera: Nenda zako bwana! Huwezi kukionja hicho cheo unachokitamani ... Nenda! Unasita nini (uk. 11).

Maneno ya Rais Kapera kwa waziri wake ni kejeli inayotashtiti. Kwanza alimuuliza swali lililokosa jibu. Papo hapo anamwambia alambe pua yake,

kitendo ambacho hakiwezekani. Kisha, anamfukuza na kumwambia maneno makali. Hilo ndilo lengo alilokuwa amekusudia. Rais Kapera alifanya hivyo kwa makusudi ili kumuadhiri. Kejeli hii ina nafasi ya kumjeruhi na kumuadhiri mkosaji.

Aidha, Rais Kapera anamkaribisha Waziri wa Ulinzi kwa maneno ya inda, tashtiti na jejeo, ingawa anajaribu kutumia lugha tamu inayoficha hasira zake. Baada ya makaribisho hayo yaliyoonekana kama ni ya wema, waziri huyo alielewa kuwa makaribisho hayo yalikuwa ya kejeli na yamebeba shari, kama inavyoonekana katika dondoo hili: “Karibu Bwana Mkubwa! Waziri wa Ulinzi! Mkuu wa nchi hii! (*Waziri anashindwa kukaa. Rais Kapera anavua miwani na kuiweka mezani*)” (uk. 8). Kauli hii inaonekana inakinzana na hali halisi iliyopo. Lugha iliyotumika inaonesha hali ya uhusiano wa karibu; maneno yanaashiria pongezi lakini toni ya sauti iliyotumika na matokeo ya kauli hiyo inadhihirisha kejeli. Rais Kapera anamshambulia Waziri wa Ulinzi kwa maneno mabaya ya kashfa, na baadaye anamfukuza, hali inayokinzana kabisa na maneno yaliyotumika katika makaribisho aliyopewa. Matumizi haya ya kinaya cha kitashtiti ni ishara ambayo ni tata na changamano, kwa kuwa na ukaribu chanya na wakati huohuo ukaribu hasi. Kejeli hiyo imetumika kwa lengo la kumsimanga na kumuadhiri muovu huyo.

Pia, kejeli nyingine imebainika kupitia mazingira ya jela. Jela kunaonekana kuna wafungwa wengi. Kila mfungwa anaonekana anafanya juhudi ya kuangalia nje kupitia tundu walilotoboa. Hii ni ishara kuwa wana hamu kubwa ya kutaka kuona nje kutokana na kifungo cha muda mrefu (kur. 1-8). Hali inayoashiria uvunjifu wa haki, lakini wakati huohuo Rais Kapera na mawaziri wake wanadai kuwa wako katika safari ya kutafuta nchi ya usawa, haki na demokrasia ilhali mkulima akiwa amefungwa kitambaa cheusi usoni, na kuwekewa ulinzi mkali. Mkulima huyu haruhusiwi hata kuuliza ama kusema kitu chochote (kur. 27-38). Ukinzani huu wa matukio unaojitokeza katika muktadha huu ni kejeli yenye kudhihaki kauli ya Rais Kapera. Rais huyo ni kielelezo cha wanaohubiri usawa na demokrasia, wakati huohuo, wale wanaodai demokrasia amewaweka kizuizini; anawapa



vitisho kwa nia ya kuwanyamazisha. Katika kutetea hoja hii Simon (2014) anaeleza kuwa safari ya mzunguko inayoongozwa na Rais Kapera ya kuufikia usawa, haki, ukweli na demokrasia inaonekana kutokea sanjari na kufungwa gerezani kwa wanaharakati wanaopigania ukweli, haki, demokrasia na kupinga uigaji, na ambapo hali hiyo inaakisi hali ya uongozi wa Rais Kapera. Sasa tujiulize, hiyo safari ya kufika katika nchi ya usawa na demokrasia, chombo chake cha kusafiria kitapatikana? Kweli katika hali kama hiyo, kitawafikisha walikokusudia? Kejeli hii ina lengo la kukosoa uozo wa aina hiyo.

Kejeli nyingine zinazotashtiti hali ya uvunjifu wa haki na demokrasia zilizo na ucheshi zinatumiwa tena katika dondoo lifuatalo (kur. 29-30:

Rais Kapera: Unaweza kutueleza njia ya kwenda nchi iitwayo Usawa?

Jitu: (*Kwa mshangao*) Usawa! Au labda unatania, (*Kimya*)

Sidhani kama mtafika huko wakati wa uhai wenu. Hata robo tu ya njia bado!

(*Akiwatazama mawaziri*) Na hawa vilevile! au wanatania!...

Korchnoi Brown: ... kabla ya kuondoka katika nchi hii itabidi kupambana na majitu yanayofanana na mimi. Mkitoka hapo mtafika katika njia nyembamba (*Akiwaonesha mawaziri*) hawa hawatapita hawa! ... Kutoka Fraternalite mtafika Usawa. Ulizeni tu watu watawaonyesha! Mkifika usawa mtawakuta Waswahili wenzenu wameketi nje ya ikulu ndogo ya Revensto (kur. 29- 30).

Dondoo hili linaonesha hali ya wasiwasi wa kufika katika safari ya kuelekea nchi ya Usawa, hasa kwa mawaziri wa Rais Kapera. Tunaporejelea msimbo wa kiseme, elementi nasibishi zilizotumika zinatupa picha inayoashiria kuwa mawaziri hao walikuwa wasaliti. Ingawa wamo katika safari ya kuelekea katika usawa na demokrasia, matendo yao yanadhihirisha kuwa hawakuwa tayari kutekeleza masharti ya safari hiyo, yaani mfumo wa siasa ya ujamaa alioupigania Rais Kapera kwa faida ya umma mzima. Kauli anayoitoa Jitu inayosema, "... Mkitoka hapo mtafika kwenye njia nyembamba" ni sitiari inayomaanisha kuwa, usawa na demokrasia ni vitu

visivyoweze kana kufikiwa katika serikali ya Rais Kapera. Yumkini, hali hiyo ya masikitiko ya Rais Kapera na matumbo makubwa ya mawaziri hao ni ishara ya ufisadi. Hii ni tashtiti inayokosoa tabia hiyo ya usaliti na ufisadi katika jamii.

Mwandishi pia anakejeli kwa kutumia njia ya ucheshi, kuonesha fikra za viongozi katika kuleta mabadiliko katika nchi. Mabadiliko katika nchi ya Rais Kapera ni ya kushtukizwa. Ingawa mabadiliko katika nchi ni ishara njema, Rais Kapera hakufanya uchunguzi makini na wakutosha, kuleta mabadiliko hayo. Pia, kulikosekana ushauri. Kilichofanyika ni kuwa, mawazo ya watu wachache katika nchi ndiyo yaliyotumika katika kuleta mageuzi. Hali hiyo inaonekana katika dondoo lifuatalo:

Rais Kapera: ... ninapotazama hali ya watu wangu ... moyo unaniuma! moyo unaniuma! ... nimekuwa nikifikiria, tena kwa muda mrefu sana ... Watu!

Nimekuwa nikifikiria njia ya kuwaondoa katika hali hii ya dhiki ... ili kutafuta suluhisho nikaanza kuwa na tabia ya kusomasoma . . . Mara nikasikia sauti moyoni na mawazoni “Rais Kapera! Vaa kaptula hilo kwa uaminifu. Waondoe watu wako katika unyonge na umasikini. Nimekata shauri kulivaa. Sasa nataka wewe uniambie kama linanitoshia, kabla watu wengi nchini hawajaniona nalo (uk. 15).

Kauli za Rais Kapera zinaonekana ni kinyume na lengo la kaptula alilolivaa. Mwandishi anatumia ucheshi kukejeli hali anayoizungumza na jinsi inavyokinzana na matendo ya Rais Kapera katika jamii hiyo, kwani ule uaminifu aliotakiwa afanye hauonekani katika utendaji wake. Mawazo ya Rais Kapera ya kulivaa kaptula kwa uaminifu yanaonekana yalizingatia zaidi utashi binafsi. Raia wanaonekana wanalalamika kuwa hawatendewi haki. Lakini kwa kuwa wazo la kuvaa kaptula lilimtokea Rais huyo katika mawazo yake, aliamua kulitekeleza bila hata ridhaa ya walio wengi na wengine kubakia wakiburuzwa tu. Kwa mfano, katika uk. 12 Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje anaonekana anafuata mkumbo tu. Anabaki kulisifia

kaptula ilhali anaona matatizo ya kaptula alilovaa Rais Kapera. Hii inaashiria ukosefu wa demokrasia. Kama inavyooneshwa kupitia Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje (uk. 12), “Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje anamweleza tarishi: “... Wewe katika bara hili usijaribu kusema ukweli! Utakuja kujutia ulimi wako!” (uk. 12). Kauli hiyo inaonesha namna mwandishi anavyotumia kejeli ya kitashtiti kuonesha ukandamizwaji wa mkulima. Hivyo, tashtiti hii imechukua nafasi muhimu ya kuyacheka, kuyabeza na kuyahakiki matendo maovu ya jamii. Dhima hii haitofautiani na namna inayoelezwa na Wamitila (2010) anaposema: “tashtiti katika fasihi au usemi huchochewa na mazingira ya ukandamizaji”. Msanii au mwandishi anaihakiki jamii, matendo yake, mielekeo yake matarajio yake na ndoto zake, na kutoa kauli inayoishia kuufichua uozo. Hivyo, kauli zilizotumiwa na mwandishi katika dondoo hili, lengo lake ni kuizindua jamii na kukosoa utawala na uongozi wa Rais Kapera, ambapo kwa mujibu wa jicho la kihakiki anaona unakwenda kinyume na maadili yaliyotazamiwa katika jamii hiyo, yaani jamii yenye haki, usawa na demokrasia.

Katika kushadidia hoja hii Simon (2014) anasema, Kezilahabi anawavalisha Rais Kapera na mawaziri makaptula ambayo yanawafanya kuwa vichekesho kwa nia ya kuonesha kuwa viongozi hawa wa Kiafrika wanafuata falsafa ya uongozi ya Ujamaa wa Kiafrika wasiouelewa. Nchi zilizopata uongozi baada ya miongo mitano ya uhuru, bado hazijafikia ukweli, usawa, haki, demokrasia na ufanisi ulioahidiwa na viongozi. Ingawa ujamaa na kujitegemea bado ndiyo falsafa na dira ya nchi inayozungumziwa, siasa hii bado inawapeleka wananchi katika safari ndefu ya mzunguko isiyoleta mazao wala manufaa yoyote.

Kejeli nyingine inayoakisi mtazamo huu inapatikana kupitia wafungwa. Kwa mfano, wafungwa 1- 6 walionekana wanakumbana na adhabu ya kifungo baada kupinga anayoyataka Rais Kapera. Maelezo ya Rais Kapera yanathibitisha suala hilo kama ifuatavyo:

Rais: Kapera: ... kazi nzuri, kazi nzuri, (*Kimya*). Vipi wale panya tuliowaweka huko jela!

Waziri wa Mambo ya Ndani: Kwa muda wa miaka tisa iliyopita hatujawaruhusu kutoka nje. Habari nilizo nazo ni kwamba akili zao zinaanza kuwa butu (uk. 9).

Dondoo hili limetumia mazingira magumu na ya kukatisha tamaa. Tunaporejelea msimbo wa kiurejelezi, viashiria vya utamaduni vilivyotumika vinatuonesha uhalisi wa jamii zetu. Jamii zenye mwenendo wa kutumia visasi na kuwakomoa raia wengine kutokana na utashi wao. Jamii zinazoshindwa kujenga umoja na mshikamano na kusameheana. Viashiria hivyo vinatoa picha inayoonesha kwa uwazi baadhi ya sababu za watu hao kufungwa kuwa ni kutokana na ubinafsi. Ingawa mwandishi anatumia utawala wa Rais Kapera, kinacholengwa hapa kinaihusu jamii yote. Isipokuwa Rais Kapera ametumika kama msingi wa utamaduni uliozoeleka ndani ya jamii. Kejeli iliyotumika hapa, inalenga kukaripia tabia hiyo na kuufichua uozo huo ili kuifanya jamii izinduke na iweze kujirekebisha.

Risala ya wafungwa (kur. 21-24) ni kielelezo kingine kinachothibitisha kejeli inayotashtiti ubabe wa uongozi katika bara la Afrika. Risala inaonesha namna ‘wahalifu’ walivyokamatwa na kuingizwa jela. Wafungwa walipewa adhabu hiyo kutokana na kufanya maandamano ya kupinga vitendo vya viongozi wa nchi huru za Kiafrika. Rais Kapera na mawaziri wake ni mawakili wa viongozi wa aina hiyo. Kwa mfano, namna viongozi wanavyojiongezea mishahara mikubwa na marupurupu mengi wakati wananchi wanaonekana wamo katika shida kubwa. Malalamiko hayo yanaonesha ukinzani uliopo kati ya uhalisi wa maneno ya Rais Kapera ya kuanzisha siasa zake na matokeo yake kwa raia. Hivyo, ni wazi kuwa mwandishi ametumia kejeli kuihadharisha jamii kuwa makini na kauli za baadhi ya viongozi.

### 1.6.2 Nafasi ya Kejeli katika Muktradha wa Kiuchumi

Suala la uchumi pia limebainishwa katika tamthilia ya *Kaptula la Marx* kupitia muktradha wa jela. Uchumi imara ni nguzo muhimu ya maendeleo ya nchi yoyote duniani. Nchi zilizo chini kiuchumi huwa chini kimaendeleo. Kwa mfano, nchi nyingi za Kiafrika uchumi wake uko chini kutokana na uduni wa maendeleo. Mwandishi ameionesha hali ya Afrika kiuchumi na namna mataifa hayo yanavyopitia vikwazo vingi kutokana na mfumo wa uchumi duniani. Hali hiyo inaoneshwa kupitia wahusika wafungwa wakati walipokuwa wanachungulia kwenye tundu walilolitoboa ili waone namna ulimwengu ulivyo huko nje baada ya kufungiwa kwa siku nyingi. Mfungwa Na. 6 alipochungulia alidai kuwa ameona Wazungu wengi. Dondoo lifuatalo linadhihirisha hali hiyo:

- Mfungwa 6: Lo! Si Wazungu hao! Wengi ajabu!
- Mfungwa 1: Labda Waisraeli!
- Mfungwa 6: (*Akitazama kwa uangalifu zaidi*) Mmoja wao kama Hitler! Haikosi ni ndugu yake! (*Akiendelea kutazama*) Wote wameenea mikoba ya fedha! Mikoba yao imeandikwa “Benki ya Dunia”
- Mfungwa 2: Wametuletea fedha au wamekuja kuchukua! Watazameni vizuri.  
Wameshibashiba kidogo au wana njaa!
- Mfungwa 6: (*Akiendelea kutazama*) Matumbo yamevimba, lakini meno yao kama mbwa vichaa wenye njaa!
- Mfungwa 1: Basi hiyo ni shibe ya ugonjwa! (uk. 6).

Kejeli katika tukio hili ziko wazi kwa sababu kinachoelezwa ni kinyume cha maana na hoja zilizotumika. Mwandishi anatumia Wazungu kuashiria mataifa makubwa. Pia, anatumia Hitler kuonesha kuwa ni mtu mwenye uchu wa kutawala. Ingawa Hitler alitaka kuitawala dunia kisiasa, lakini ingelikuwa vigumu sana kuitawala bila kuzitawala nchi hizo kiuchumi. Hivyo, mwandishi anatumia kejeli kutashtiti na kuonesha kwamba, Mzungu aliyemuona kama Hitler, na wale waliovaa mikoba ya fedha iliyoandikwa Benki ya Dunia ni mataifa makubwa yanayozinyonya nchi za Afrika.

Tukirejelea msimbo wa kirejelezi, viashiria vya kiutamaduni vilivyooneshwa katika dondoo hapo juu vinatufanya kuunda uhalisi unaotuwezesha kufasili kuwa, mataifa hayo makubwa ndiyo yanayomiliki benki hiyo na pesa nyingi. Wakati huo, mataifa yanayoendelea, huishia kuwa tegemezi na yenye madeni tu kutokana na mikopo yenye masharti magumu wanayopewa na mataifa hayo makubwa.

Mwandishi anapowasawiri Wazungu hao kuwa na matumbo yaliyovimba, tunaweza kuhusisha msimbo wa ishara na jazanda hiyo, kuashiria ulafi wa mataifa hayo makubwa dhidi ya mataifa ya Kiafrika. Pia, anaposema, “meno yao yako nje kama mbwa kichaa” inaashiria hali ya kutotosheka. Siku zote wao hujiweka tayari kwa kutumia hila yoyote ile, kuendelea kuinyonya Afrika na kuitawala. Kama ilivyo kwa mbwa kichaa, ambaye huwa hachagui yeyote yule atakayempitia mbele yake, kwani humfukuza na kumdhuru. Hivyo ndivyo hao nao walivyo, kwani wako tayari kuwadhuru Waafrika kwa visingizio vya misaada na mikopo. Misaada yao ya kibenki na mengineyo mara nyingi huleta madhara ya kiuchumi na kijamii kwa bara la Afrika. Pia, mwandishi anaonesha kuwa mbali ya Benki ya Dunia, mbinu nyingine ya kibepari inayotumiwa na mataifa hayo makubwa ni kupitia Soko la Dunia. Katika muktadha huu mwandishi anakejeli kwa kuita ‘Jela.’ Jela ni sehemu inayotumika kumuweka mtu katika kifungo. Kwa maana hiyo, anakuwa hayuko huru na wala hana maamuzi. Hubakia kuwa ni mtu wa kutii amri atakazopewa na askari wa jela. Hali hii inadhihirika katika dondoo lifuatalo:

- Mfungwa 6: (*Anaendelea kutazama. Kwa mshangao*)  
Ala! Huko nje naona jela nyingine tena!
- Mfungwa 1: (*Kwa kujituliza*) Kumbe wafungwa tuko wengi ulimwenguni.
- Mfungwa 5: (*Kwa mshangao*) Jela kuwa soko tena!  
Labda ni soko kweli! Tazama vizuri,  
pembeni hakuna soko la Afrika? ... (uk. 6).

Mwandishi anatumia neno ‘jela’ kuashiria Soko la Dunia ambalo linaendeshwa katika mfumo wa kibepari na kiunyonyaji. Mfumo huo

umehodhi biashara ya ulimwengu. Matokeo yake ni kuifanya Afrika kukosa sauti ya kujitetea kiuchumi, kwani bidhaa za Afrika hupangiwa bei na mataifa makubwa ingawa wao ndio wazalishaji. Pia, mara nyingine hujitokeza tatizo la kushushwa bei kiholela kwa bidhaa hizo za Afrika ili mataifa hayo makubwa yaweze kujinufaisha zaidi kiuchumi. Hoja hizi zinaafikiana na mawazo ya Simon (keshajatwa) anayeeleza kuwa, kwenye muktadha huu, Wazungu wanaowakilisha ‘Benki ya Dunia’ na ‘Soko la Dunia’ ni ishara ya ukoloni mamboleo ambao unadhibiti uchumi na biashara ya nchi za Afrika. Nchi hizi zinaingia katika jela ya kudaiwa na kulimbikiziwa madeni yasiyomalizika. Wazungu wanaorejelewa hapa wamevimba matumbo na meno yao yako nje kama mbwa vichaa wenye njaa – ili kuashiria uchoyo, ulafi na tamaa waliyo nayo. Mbwa vichaa wenye njaa ni taashira kwamba Wazungu ni wahusika hatari kwa nchi za Kiafrika kama vile mbwa kichaa walivyo hatari kwa binadamu. Hali hii huliweka bara la Afrika katika uchumi duni. Katika mfumo huo, bidhaa za Afrika hununuliwa zikiwa bado ni malighafi. Baadaye, malighafi hizo huzalishwa bidhaa ambazo huletwa kuuzwa tena Afrika kwa bei ya juu. Hali hii hulifanya bara la Afrika kuwa katika ufungwa wa kiuchumi, kutokuwa na sauti zaidi kiuchumi kutokana na kuwa tegemezi. Mawazo haya yanaafikiana na mawazo ya Rodney (1973) anayeeleza kuwa Wazungu ndio waliokuwa na nguvu za kutoa maamuzi ndani ya mfumo wa biashara wa kimataifa. Ufafanuzi mzuri kabisa wa suala hili unatokana na ukweli kwamba kile wanachokiita sheria za biashara za kimataifa ambazo zimetawaliwa na mwenendo wa taifa katika bahari kuu si chochote bali ni sheria za Kizungu za kuikandamiza Afrika. Afrika haikushiriki katika soko lake lenyewe, na katika mifano mingi Waafrika walikuwa ni waathirika/wahanga, kutokana na sheria zilizowatambua wao kama ni bidhaa zinazosafirishwa. Mbali ya yote hayo, nguvu za kufanya maamuzi ya Wazungu yaliyofanywa yalikuwa ni kuwachagulia Waafrika kitu gani lazima wakisafirishe ili kukidhi mahitaji ya Wazungu (Rodney, 1973).

Kwa ujumla, madondoo hayo yamejengwa kikejeli. Mwandishi anatumia kejeli hizi kimzaha na kiubwege kwa kuwavika wahusika wake uhusika wa kuwa kama watu wasioelewa kitu. Wamo katika mshangao kwa kile

wanachokiona. Wanashangaa na kuuliza maswali mengi ambayo hayana hata majibu. Kila mmoja wao alishangaa au aliuliza, na hakuna hata mmoja kati yao aliyepata jibu la swali lake wala ufafanuzi wa kilichomshangaza. Mwandishi anatumia njia hii kuukamilisha ubwege. Kejeli hizi zinalenga kufikirisha hadhira ili waweze kutafakari vyema kuhusu ujanja na ubaya wa mataifa makubwa yaliyoendelea kwa nchi za Afrika.

### **1.6.3 Nafasi ya Kejeli katika Mukadha wa Utamaduni**

Utamaduni ni dhana pana. Hata hivyo, katika makala hii utamaduni unazigatiwa kuwa ni masuala ya mila, desturi, sanaa na maadili ya jamii. Vilevile, katika tamthilia hii, mukadha wa utamaduni umebainishwa kupitia ripoti ya Waziri wa Utamaduni wa zamani. Kejeli imejitokeza wakati alipotakiwa aeleze maendeleo ya wizara yake ya mwaka. Kejeli hiyo inadhihirishwa na dondoo lifuatalo:

Timu yetu ya taifa imetolewa na timu ya taifa ya jirani zetu. Kuhusu mambo ya kale, tumetoa pesa kutengeneza upya mapango ya watu wa kale, wataalamu wetu wanaendelea kuchimbua mafuvu. Kuhusu mila, hivi sasa tunafanya uchunguzi juu ya matumizi ya nyoka katika ngoma, uchawi na talaka. Kuhusu lugha, wananchi wameonesha kuwa na mwamko mkubwa kisiasa. Wanaimba ngonjera na mashairi juu ya ujamaa, tena yenye vina. Ni hayo tu Mtukufu Rais (uk. 10).

Pia, katika mwendelezo wa ripoti ya Waziri wa Utamaduni kejeli iliyobainika ni ya kidhihaka. Hii ilitokea pale Rais Kapera alipomuuliza Waziri wa Utamaduni maswali wakati alipomwita ofisini kwake ili kueleze maendeleo ya wizara yake. Kabla ya kumaliza kueleza, alimtupia swali la kumuumiza kwa kumkejeli kuhusu vitendo vyake viovu. “Je, kutembea na wake za watu nao ni utamaduni!” (uk. 11). Katika mfano huu, mwandishi anatumia kejeli ya kidhihaka. Kejeli hii ina sifa ya kuumiza. Wamitila (2008) anashadidia kwa kusema kuwa kinaya cha aina hii kimejengwa kwenye uhusiano wa karibu kati ya kinaya na dhihaka. Dhihaka hukusudia kukera, kuudhi na kumletea mlengwa hisia fulani ya kubezwa au



kudharauliwa. Kinaya ya aina hiyo haimaanishi tu kinyume, bali pia inakusudia kukera, kukosoa au kumuudhi anayezungumziwa. Vilevile, mzungumzaji hutumia kejeli hiyo kwa lengo la kumjuza mhusika kuwa analolifanya tayari linajulikana. Mzungumzaji hutumia fursa hiyo kama njia ya kumuonya mhusika.

Unapoliweka swala hili katika msimbo wa kiurejelezi, swali lililoulizwa kama, “kutembea na wake za watu nao ni utamaduni”, linatuundia uhalisi mahususi wa mwandishi juu ya mtazamo wake kuhusu maadili ya viongozi. Inawezekana kuwa aliuliza swali hilo kwa kusudio maalumu, ambapo tukio hilo ni kinyume na matarajio ya mwandishi. Mtazamo wake ni kuwa kiongozi hapaswi kuwa ni kinara wa uvunjaji wa maadili. Hivyo, mwandishi ametumia kejeli hiyo kudhihaki, akiitaka hadhira yake kufikiria kwa nini mwandishi ametumia swali hili. Je anaashiria nini?. Kejeli hii inadhihaki tabia hiyo mbaya inayofanywa na baadhi ya viongozi ambao walitakiwa kuwa mfano mzuri kwa jamii zao. Pia, anakebehi na kuionya hadhira yake, na kuwahadharisha viongozi juu ya umuhimu wa kuwa na maadili njema. Kwani ikiwa kiongozi ana tabia mbaya kama hiyo atawezaje kuwakemea anaowaongoza katika maadili ya jamii yake?. Kebehi aliyotumia mwandishi inalenga kuikosoa jamii.

#### **1.6.4 Nafasi ya Kejeli katika Mukstadha wa Kijamii**

Kupitia tamthilia hii, pia mwandishi anatumia kejeli kuonesha ukiukwaji wa haki na upendeleo unaofanyika katika vyombo vya sheria kama vile mahakama. Katika mukstadha huo wa mahakama ya kubuni iliyoundwa na wafungwa, Mfungwa 6 anazungumza kikejeli kwa kudai kuwa nje hakuna haki tena na haki inapatikana jela. Alipania kuionesha haki inayotendeka jela. Dondoo lifuatalo linatudhihirishia maelezo hayo:

- Mfungwa 6: Huko nje hakuna tena haki!  
Mfungwa 5: Isipokuwa humu jela!  
Mfungwa 4: Na tuoneshe basi hiyo haki. (*Anapiga magoti mbele ya mfungwa . . .*) Huyu ndugu

- anashitakiwa kwa kosa la kuiba mkate kwenye duka la Mhindi.
- Mfungwa 6: Unakiri kosa?
- Mfungwa 2: Ndiyo lakini nilikuwa na njaa.
- Mfungwa 6: Jela miaka kumi na viboko 25 . . .
- Mfungwa 1: Huyu anashtakiwa kwa kosa la kuiba pesa za shirika la ndege, kiasi cha shilingi milioni ishirini na moja
- Mfungwa 6: Unakiri kosa!
- Mfungwa 3: Ndiyo, nakiri.
- Mfungwa 6: Jela kwa muda wa siku moja! . . . (uk. 24).

Dondoo hili linajenga kejeli ya kitashtiti. Mwandishi anatumia mtindo huu wa tashtiti ya ufyosi kudhihaki mambo ya msingi ya kimahakama. Kama anavyoshadidia Wamitila (2008), ufyosi ni mtindo wa kitashtiti katika uigizaji, ambapo mambo ya dhati yanadhikiwa kwa kuzungumziwa kiubwege na ya kipuuzi; yanawekwa kama hayana umuhimu mkubwa. Katika mfano huo, mwandishi anaonesha namna gani anavyokejeli mchezo unaochezwa katika mahakama, namna mwenye cheo na wadhifa anavyohukumiwa na mnyonge anavyohukumiwa. Aidha, inaonesha jinsi aliye na kosa kubwa anavyopendelewa na aliyefanya kosa dogo alivyopewa hukumu kubwa. Hali hiyo inaonesha ubaguzi wa kitabaka kati ya wenye vyeo na watu wa chini. Hii ni kejeli inayosuta ufisadi uliopo wa baadhi ya vyombo vya sheria na baadhi ya wanasheria ambao haki huifanya batili na batili huifanya haki. Mwandishi ametumia mtindo huo kwa lengo la kubeza hali hiyo.

Pia, mwandishi anaonesha kuwa katika nchi huru za Kiafrika bado kuna jamii zinazokosa huduma muhimu za kijamii. Kwa mfano, kukosa elimu kuanzia elimu ya awali, ambayo inamuwezesha mtu angalau kusoma na kuandika lugha yake. Wanajamii kukoseshwa elimu ni kukaribisha ujinga. Elimu ndio msingi wa kila kitu katika maisha. Taifa ambalo litakuwa halina raia walioelimika litaishi katika maisha yaliyojaa kiza. Mwandishi

amemtumia mhusika Mfungwa 5 kama kielelezo cha watu waliokosa elimu katika jamii. Kwa mfano, hali hii inajieleza katika uk. 4:

- Mfungwa 5: Mimi sijui kusoma. Nitawaonesha tu alama kwa mkono
- Mfungwa 4: Subiri nichukue kalamu yetu
- Mfungwa 5: Naanza (*Anafananisha herufi hewani kwa Mkono hali akitazama tunduni – Mfungwa 4 anaandika*)
- Mfungwa 4: (*Kwa sauti ya juu*) CHAMA!
- Mfungwa 5: (*Kwa mmako*) Nini! Hilo ni jina langu la ujambazi! Yaani kati ya majambazi yote huko nje jina langu ndilo bado linajulikana.
- Mfungwa 5: (*Bado anaendelea kuandika herufi hewani*)
- Mfungwa 4: CHAMA CHA UJAMAA WA AFRIKA (*Wote wanatazamana isipokuwa Namba 6 hawajui maana yake*) (uk. 4).

Kauli alizozitumia mwandishi zina lengo la kukejeli na kuonesha hali ya jamii hiyo ilikosa elimu na mwelekeo. Mfungwa 5 anathibitisha kuwa hajui kusoma na kuandika. Lakini huyo aliyejaribu kuandika anaandika tu na kusoma kikasuku kwa kufuata maumbo ya sauti ilhali hajui hata ni nini; hali hii inaashiria ujinga. Pia, maelezo ya Mfungwa 5 yanadhihirisha kutokujielewa kwao. Kwa mfano, Mfungwa 5 anaonesha kuwa hata sababu ya kufungwa kwake haelewi. Haelewi pia kama kufungwa kwake jela ni njia ya kumfunza, yaani kuacha tabia ya ujambazi iliyomfikisha jela. Maelezo yake hayaonekani kuwa ni ya mtu anayejutia matendo aliyoyafanya alipokuwa uraiani. Anaonekana anafurahia na kujigamba. Hii ni hali ya kutojitambua. Mwandishi anatashtiti hali hiyo na kudhihirisha kejele katika mambo wawili. Kwanza, mfumo wa magereza ya Afrika. Pili, mfumo wa elimu na mwelekeo wake kwa jamii, kwani katika kundi lote hilo aliyeonekana ana mwelekeo ni mtu mmoja tu, Mfungwa 6. Katika muktadha huu, ni wazi kuwa mwandishi anakosoa hali ya elimu kuwa bado ni duni.

## 1.7 Hitimisho

Makala hii inahitimisha kuwa mbinu ya kejeli ina umuhimu mkubwa katika uandishi wa tamthilia. Ingawa jamii imezoea kuiangalia kejeli katika mtazamo hasi, katika uandishi wa kazi za fasihi, kejeli ina dhima sawa na mtazamo wa kifalsafa wa kumtaka mtu ajitambue. Hivyo, kejeli zina nafasi muhimu na maalumu zinazosimamia katika miktadha tofauti. Nafasi hizo ni kujenga umakini na tafakuri kwa pande zote mbili; upande wa fanani na hadhira. Aidha, nafasi nyingine ni kufichua uozo unaofanyika katika jamii na kuikumbusha hadhira juu ya mambo yaliyomo katika jamii zao. Husuta, hukosoa na huhadharisha juu ya suala la uongozi na uzalendo wa kweli kwa wanajamii. Vilevile, hukemea mambo yasiyo na faida kwa taifa, kama vile ufisadi, ubaguzi, unyanyasaji na kutibu uozo huo. Huwazindua na kuwaonesha raia njia sahihi za kujenga taifa lao. Huwadharau na kuwakebehi wale wanaofanya uharibifu na wasiojitambua miongoni mwa raia. Pia, huyaweka wazi matatizo na changamoto mbalimbali ndani ya jamii ili kutafutiwa ufumbuzi na kuondoa changamoto hizo katika nchi zao. Hujenga uwezo wa kufikiri na kuchambua mambo ndani ya jamii zao kwa faida ya nchi zao. Pia, kejeli hutumika kuburudisha jamii, hususani zinapotumia mbinu ya ucheshi. Mbinu ya kejeli ni silaha nzuri ya kiuandishi. Matumizi yake yana tija kwa wasomaji na jamii kwa ujumla kutokana na nguvu za ziada za kuifikirisha na kuimulika jamii kwa njia ya kufurahisha.

## Marejeleo

Baldick, C. (2008). *The Consise Dictionary of Literary Terms*. (4<sup>th</sup> Eddition). London: Oxford University Press. kutoka DOI: 10.1093/acref/9780199208272.001.0001.

Cuddon, J. A. (1991). *Dictionary of Literary Terms and Literary Theories*. Clays Ltd: St Ives plc.

- Dib, F. Z. (2019). *The absurd and irony in Samuel Beckett's Waiting for Godot and Eugene Ionesco's The Lesson*. [master dissertation, University of Oum ElBouaghi]. (hajachapishwa)dib.univoebidz:8080/jspui/bitstream/123456789/8976/1/ABSURD%AND%IRONY%20IN%WAITING%20FOR%GODOT%20AND%THE%20LESS.
- Grisworld, C. L. (2002). Irony in the Platonic Dialogue. *Journal of Philosophy and Literature*. Vol 26. (1), 84-106.muse.jhu.edu/article/2106/pdf. 23/6/2019. <http://doi:10.1353/phl.2002.0012>
- Highet, G. (1962). *Anatomy of satire*. New Jersey, United State: Princetone University Press, [googlebook.google.co.tz/book/aboutAnatomyH\\_of\\_satire.html?id.12/8/2019](http://googlebook.google.co.tz/book/aboutAnatomyH_of_satire.html?id.12/8/2019).
- Frey. N (1990). *Anatomy of Criticism*. Four Essays. London: Penguin Books.
- Kezilahabi, E. (1999). *Kaptula la Marx*. Dar es Salaam: DUP Ltd.
- Khatib, M. S. (1986). Tamathali za semi. katika *MULIKA 18*, (Wah). Mdee, J. S. na Mbogo.. Dar es Salaam: TUKI.. (kur 1-15).
- Kierkegaard, S. (1977). *Concept of irony*. *Academyofidea.com* /2020/10/soren-kierkegaard-despair 20/05/2020.
- Mbatiah, M. (2014). Satire and the theme of victims and culpritis in *Miradi Bubu ya Wazalendo*. *Jarida la Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili*, Vol. 77, uk. 148 – 159.
- Mrikaria, S. M. (2010). Kejeli na Fasihi ya Kiswahili. katika *KISWAHILI FORUM* Vol. 17. Uk. 104-125. [ul.qucosa.de/api/qucosa%3A11481/attachment/ATT-0/](http://ul.qucosa.de/api/qucosa%3A11481/attachment/ATT-0/)
- Muecke, D. C. (2018) “Irony and the Ironic”. 2 Park Square, Milton Park, London: Routledge. From

<http://doi.org/104324/978131588342.eBook> ISBN (12July2017)  
(First Pub.1970). Methuen & Co. Ltd.11New Fetter Lane.

- Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuu Vikuu*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.
- Ponera, A. S. (2014). *Ufutuhi katika nathari ya Kiswahili ya: Ulinganishi wa nathari za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi* [Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika Sanaa, haijchapishwa]. Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Rodney, W. (1973). *How Europe Underdevelop Africa*. London: Bogle-L'Ouverture Publications. Kutoka <http://www.marxists.org/subject/africa/rodney-walter/how-europe/ch03.htm>. 22/05/2019.
- Sedgwick, George (1935). *Of Irony, especially in drama*. Ontario, Toronto, Canada: University of Toronto Press. [achieve.org/details/in.ernet.dli.2015.5013/page/n101/mode/2u](http://www.achieve.org/details/in.ernet.dli.2015.5013/page/n101/mode/2u)
- Simon, K. B. (2014). *Ishara katika Kaptula la Marx na Kijiba cha Moyo: Mtazamo wa Kisimiotiki*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijchapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.
- Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Limited.
- Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.
- Wamitila, K.W. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi na Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: Muwa Publishers limited.
- Wilson, D., & Sperber, D. (2012). *Explaining irony; Meaning and Relavance*. Cambridge, United Kingdom: Cambridge University Press. Kutoka Doi:<https://doi.org/10.1017/CB09781139028370.00>